Maswali

1. Nani aliumba kila kitu?
2. Jina la bustani yenye Mungu alitengenezea Adamu na Hawa iliitwaje?
3. Majina ya miti miwili iliyokuwa katikati ya bustani iliitwaje?
4. Mungu aliamrisha Adamu asifanye nini?
5. Rafiki wa kipekee mwenye Mungu alitengenezea Adamu alikuwa nani?
6. Nyoka aliambia Hawa nini?
7. Adamu na Hawa waliasi Mungu namna gani?
8. Adhabu kuu ilikuwa nini?
9. Mbona Adamu na Hawa waliondoka bustani?
10. Adamu na Hawa walipewa ahadi gani ya tumaini?

Majibu

1. Mungu
2. Bustani ya Edeni
3. Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu na Mti wa Uzima
4. Lazima asikule tunda la Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu
5. Hawa
6. “Hautakufa. Utakuwa na hekima.”
7. Walikula tunda walilokatazwa na Mungu wasikule
8. Watakufa
9. Hawakukubaliwa kukula tunda la Mti wa Uzima
10. Mtu (Yesu) atakuja na yeye ndiye atamtii Mungu na atoe uhai wake kuondoa adhabu yenye dhambi ya Adamu ilileta.

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 1

1 Bustani ya Edeni

Kwa Biblia Mwanzo 1 na 3

Kiini cha somo

Kuonyesha vile vyote alivyoviumba Mungu ni vizuri sana. Mungu ali-wapa Adamu na Hawa hivyo vizuri vyote. Lakini uasi uliwaletea Adamu na Hawa huzuni.

Somo

Mwanzoni Mungu aliamua kuumba mtu katika nchi. Alitaka amtengenezee huyu mtu pahali pazuri pa kuishi. Alifanya hewa, anga na mawingu. Tena akatengeneza bahari na nchi kavu. Mungu akafunika ardhi na nyasi, miti na maua ili ipendeze. Angani Mungu akafanya jua, mwezi na nyota kuonyesha mchana na usiku, majira na miaka. Mungu aliumba pia ndege, samaki na wanyama wa kuishi nchini.

Tena Mungu akatengenezea huyo mtu wa kwanza pahali pa kuishi pa kipekee. Akapanda bustani nzuri. Mto wa kumwagilia maji ulipita katikati. Hiyo bustani iliitwa Bustani ya Edeni.

Mungu alifanya mtu kutoka kwa mavumbi ya ardhi. Akampulizia puani pumzi ya uhai. Mtu akawa hai. Mungu akamuita Adamu. Mungu akamweka Adamu katika Bustani ya Edeni ajiburudishe na kuilinda.

Kulikuwa na kitu kimoja chenye Mungu hakutaka huyu mtu afanye. Katikati ya bustani kulikuwa na miti miwili isiyokuwa ya kawaida. Iliitwa Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu tena Mti wa Uzima. Mungu aliambia Adamu asile tunda la Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu. Akila tunda la huo mti atakufa.

Mungu alimpenda Adamu sana. Alimtengenezea dunia ya kuishi ya ajabu. Mungu alitaka kujua kama Adamu anampenda kweli kwa kutii amri moja tu.

Adamu alifurahia kukaa kwa bustani. Alicheza na wanyama na kuwapa wote majina. Lakini wanyama hawakumzungumzia. Adamu hakukuwa na rafiki wa kufanana naye. Wakati mwingine alikuwa na upweke. Mungu alitaka Adamu awe na furaha. Mungu alifanya Adamu alale usingizi mzito. Mungu akamtoa ubavu moja. Akatumia huo ubavu kumtengenezea mke. Adamu akamwita Hawa.

Adamu na Hawa walifurahia kuishi kwa bustani. Hawa alisaidia Adamu kutunza bustani. Adamu alimwambia Hawa amri ya Mungu ya kutokula tunda la Ujuzi wa Mema na Maovu.

Siku moja Hawa alienda karibu na Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu. Tunda lilionekana nzuri sana. Na kwa hiyo bustani kulikuwa na nyoka naye alikuwa mjanja kuliko wanyama wengine wote. Akaja na kumzungumzia Hawa. “Eti Mungu amesema msile tunda lolote bustanini?”

Hawa alijibu, “Tunaweza kula tunda lolote kwa bustani isipokuwa tunda kutoka kwa Mti wa Ujuzi wa Mema na Maovu. Mungu amesema tukila tunda hili tutakufa.”

Nyoka alimcheka Hawa, “Hamtakufa! Mungu amemkataza msikule kwa sababu anajua mkila mtakuwa werevu na hekima kama Yeye.” Hawa alitaka awe na hekima tena lile tunda lilionekana nzuri la kukula. Alisahahu upendo wote aliopewa na Mungu. Alitwaa tunda moja na akala. Alimwendea Adamu na akamwambia yote aliyoambiwa na nyoka. Adamu naye alitaka awe na hekima kama Hawa, kwa hivyo naye alikula lile tunda.

Bunde si bunde, baada ya kula lile tunda, wakajua kwamba wamefanya makosa. Waliaibika. Walijaribu kujifija kutoka kwa Mungu. Waliaibika kwa sababu walijua kwamba wako uchi, wakajitengenezea mavasi kutoka kwa majani ya mtini. Mungu hakufurahi kwa maana Adamu na Hawa hawakumpenda na kumtii vile.

Mungu aliuliza Adamu, “Mbona umekula tunda nililokuagiza usikule.” Adamu alijibu, “Hawa aliniambia nikule.” Hawa naye akasema, “Nyoka aliniambia nikule.”

Wote waliaibika. Nyoka aliambiwa atatambaa kwa tumbo mavumbini. Hawa atakuwa na masikitiko na uchungu wa kuzaa. Atatawaliwa na mmewe. Adamu atafanya kazi kwa jasho kwa sababu ardhi ililaaniwa ikue miiba, michongomo na makwekwe. Adhabu mbaya sana ni ile Mungu aliwambia – watakufa. Kutokea hapo Adamu na Hawa wakaanza kuwa wazazi, hatimae wakafa.

Hata kama Mungu aliwaadhibu Adamu na Hawa, aliendelea kuwapenda na akawapa ahadi ya tumaini. Mungu alisema kuna wakati atazaliwa mtu naye atamtii. Huyu mtu atarudisha watu kwa Mungu. Ataondoa hiyo dhambi iliyoletwa na Adamu. Tunajua huyo mtu ni Yesu aliyependa na kumheshimu Mungu kwa kila kitu.

Wakati mwingi tukifanya makosa tunawaumiza wenzetu. Mungu aliwatoa hizo nguo za majani ya mtini walizojitengenezea. Akaua mwana kondoo na kuwatengenezea Adamu na Hawa mavasi kutoka kwa ngozi. Mungu aliambia Adamu na Hawa kwamba wakimfanyia kosa lolote, lazima waue mwana kondoo wamletee na atawasamehe. Huu ni mfano wa Yesu. Yesu hakukosa lakini alitoa uhai wake ili Mungu atusamehe dhambi zetu.

Adamu na Hawa hawakukubaliwa tena kukaa kwa bustani nzuri. Katikati ya Bustani ya Edeni kulikuwa na Mti wa uzima. Hawakutakiwa kula huo mti kwa sababu walifanya dhambi. Walitakiwa watoke kwa Bustani ya Edeni. Mungu aliweka makerubi na upanga wa moto kuulinda huo Mti wa Uzima.